**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UCHUKUZI**

Simu : +255 (026) 2322703
Nukushi : +255 (026) 2322704
Baruapepe: km@uchukuzi.go.tz
Tovuti: https://www.uchukuzi.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba, 1 Mtaa wa Ujenzi,
S. L. P 638,
**40470 DODOMA**.

# TAARIFA KWA UMMA

## KUSOGEZWA MBELE KWA TAREHE YA MKUTANO WA KUPOKEA MAONI YA WADAU KUHUSU MAPENDEKEZO YA KUTENGENEZA KANUNI ZA USIMAMIZI WA MADHARA YA UCHOVU KWA MADEREVA ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA MWAKA 2025

***Dodoma,***
***Tarehe 18 Desemba, 2025.***

Tunawataarifu wadau wote wa sekta ya usafiri ardhini nchini kuwa, Mkutano wa Wadau kwa ajili ya kupokea maoni kuhusu mapendekezo ya kutengeneza Kanuni za Usimamizi wa Madhara ya Uchovu kwa Madereva za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za Mwaka 2025 uliopangwa kufanyika tarehe 22 Desemba, 2025 umesogezwa mbele hadi tarehe 8 Januari, 2026.

Mkutano huo utafanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Chuo cha Utalii, kilichopo Mtaa wa Shaaban Robert, Jijini Dar es Salaam kuanzia saa tatu kamili asubuhi. Tangazo hili linafuta taarifa ya mkutano wa awali iliyotolewa tarehe 9 Desemba 2025 kupitia gazeti la Mwananchi Namba 9249.

Hatua hii imefikiwa baada ya Wizara ya Uchukuzi kupokea maombi ya wadau kuwa wanahitaji muda zaidi wa kuzisoma Kanuni na kuzielewa kabla ya kushiriki kwenye mkutano.

Wizara inawakumbusha kuwa, Rasimu za Kanuni hizo zimeandaliwa kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza na zinapatikana katika Tovuti ya LATRA https://www.latra.go.tz/ na ofisi zote za Mamlaka Tanzania Bara.

Maoni ya maandishi yanapokelewa kupitia baruapepe group.maoni@latra.go.tz hadi tarehe 22 Januari 2026 ikiwa ni siku 14 baada ya mkutano.

Wote mnakaribishwa

Imetolewa na:

**KATIBU MKUU – WIZARA YA UCHUKUZI**